

HALMASHAURI YA MJII TARIME

TAREHE 12 Aprili, 2022

TANGAZO LA KAZI YA UWEKAJI MIUNDOMBINU YA MILANGO NA MADIRISHA YA ALUMINIUM JENGO LA UTAWALA HALMASHAURI YA MJII TARIME

1. Mkurugenzi wa Mji Tarime anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye ujuzi na sifa za kujenga majengo ya Serikali kuleta maombi ya kazi ya Uwekaji wa miundombinu ya **milango na Madirisha ya aluminium** katika jengo la Utawala.

2. Sifa ya mwombaji

i. Awe na Ujuzi wa Ufundi wa milango na madirisha ya aluminium.

ii .Awe mtanzania .Aambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa/Mpiga kura

iii .Awe na uzoefu wa kazi hii usiopungua Miaka 3. Aambatishe hati ya malipo au nyaraka za kazi alizowahi kufanya.

iv .Awe na ujuzi wa kusoma na kutafsiri michoro/Ramani ya Majengo.

v. Awe na uwezo wa kupata mafundi wasaidizi /vibarua na kuwalipa mwenyewe kabla hajalipwa na Halmashauri kwa kazi husika.

vi. Awe mwaminifu. Awe tayari kuwajibika kwa upotevu wa vifaa vyatya ujenzi alivyokabidhiwa eneo la ujenzi.

vii. Awe na TIN Namba.

3. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono, ipitie kwa mwenyekiti wa mtaa/kijiji/kitongoji anakoishi ikiwa na wasifu(CV) ya uzoefu wa kazi za ujenzi wa majengo ya serikali au taasisi alizowahi kufanya.

4. Pata maelekezo na ufanuzi wa kazi (Michoro na BOQ) Kutoka kwa Mhandisi wa Halmashauri ya Mji Tarime

5. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Mji, S.L.P 45 TARIME.

6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19 April, 2022 saa Tano kamili Asubuhi.

NB: ADA YA MAOMBI YA KAZI *(Signature)* HII NI TZS 10,000= (ELRU KUMI) TV

Gimbana E.Ntavyo

MKURUGENZI WA MJII TARIME

MKURUGENZI HTEBALI
KUHARIAWA